# HABARI NJEMA KWAKO NA KWA WOTE

*Ndugu,*
*tuyafikirie pamoja maisha yetu.*

## 1. HALI HALISI

*Tunatamani sana amani na heri,*
*tukizitafuta bure katika vyeo, mali na anasa;*
*kumbe mara nyingi, hata tukipata hayo, tunajisikia wanyonge tu.*

*Tunapogombania vitu tuwe navyo vingi zaidi na zaidi*
*(kama kwamba uzima wetu ungevitegemea)*
*tunajenga kuta kati ya tabaka,*
*tunaacha wengine wakose mahitaji ya msingi,*
*tunasababisha wivu, chuki na vita kati yetu,*
*hata maisha huwa yamejaa hofu,*
*ingawa tunaificha kwa kucheka na kucheza.*

*Sauti ya dhamiri inatuelekeza tutende mema, si mabaya,*
*halafu inatulaumu kwa nguvu tusipoifuata;*
*ila tukijitahidi kuwa waadilifu,*
*tunaona ndani mwetu aina ya ufa kati ya mwili na roho:*
*hivyo vinapingana kwa kutamani mambo tofauti,*
*tusiweze kufanya mema tuliyoyapanga,*
*hata tunakuja kujisikia watumwa wa dhambi.*

*Halafu tungependa kuishi daima,*
*kumbe mbele yetu tunaona mateso na kifo*
*tusivyoweza kukwepa kwa njia yoyote.*

*Tunapozika wenzetu tunapatwa na maswali mengi juu ya maisha,*
*tusielewe yana maana gani wala yanaendeleaje baada ya kufa.*

## ***2. WATU WALIVYOKABILI HALI HIYO***

*Tangu kale baadhi ya wazee wetu, wakiongozwa na Mwenyezi Mungu,*
*walimtafuta kama kwa kupapasapapasa,*
*wakamuabudu kama muumba wao na wa vitu vyote*
*na kumtolea sadaka hasa damu ya viumbe.*

*Waliweza kumtambua kwamba ni mwema kwa wote,*
*kwa kuwa anawaangazia jua lake waovu na wema,*
*na kuwanyeshea mvua waadilifu na wabaya.*

*Walipojaribu kumpendeza na kumfikia,*
*waliona kazi hiyo ni ngumu wakashindwa kuitimiza sawasawa,*
*hata wakakata tamaa na kujiachia wafuate uovu na udanganyifu.*

*Wakiogopa nguvu za giza, walitafuta njia za kujikinga nazo*
*na kuzitumia wenyewe dhidi ya wenzao,*
*hata wakatawaliwa na pepo wabaya.*

## ***3. MUNGU ALIVYOREKEBISHA HALI YETU***

*Wengi ndivyo wanavyoishi mpaka leo,*
*wasijue Mungu wetu mwenye huruma*
*alivyotufanyia katika taifa la Israeli,*
*alilojiandalia kuanzia Abrahamu, rafiki yake na kielelezo cha imani.*

*Katika uzao wake, Maria wa Nazareti, bikira mnyenyekevu,*
*alimpokea Neno wa Mungu kwa uwezo wa Roho Mtakatifu*
*akatuzalia mkombozi, Yesu Kristo.*

*Mtoto huyo wa ajabu alikua sio tu kwa umri na urefu,*
*bali pia kwa hekima na wema,*
*akijiandaa kutimiza yale yote ambayo alipangiwa na Mungu*
*na kutabiriwa na Maandiko Matakatifu*
*ya Musa, Daudi na manabii wengine.*

*Yesu alizungukazunguka nchi nzima, akitangaza haki na huruma*

*na kupenda daima watu wowote, vijana na wazee,*
*wanaume na wanawake, maskini na wagonjwa,*
*mtu aliyekwisha kuwa mwadilifu*
*na pia yule aliyehitaji kupendwa sana ili aongoke.*

*Alikuwa na furaha ya pekee kila alipopata nafasi ya kupakata watoto*
*awabembeleze na kuwabariki,*
*akisema ufalme wa Mungu ni kwa wanaofanana nao.*

*Alikuwa na maneno mazuri hasa juu ya Mungu,*
*akifundisha kumuita "Baba yetu".*

*Yesu ndiye Mwana pekee wa Mungu, ambaye alipendwa naye sana*
*na kutumwa kati yetu atuonyeshe wazi*
*jinsi anavyotupenda na kutamani tukae naye.*
*Kumbe si wote walimpokea;*
*wengine walishikilia maisha yao mabovu,*
*yaliyojaa kiburi, tamaa na unafiki,*
*wakamchukia pasipo haki wakamuua msalabani,*
*kama mtu asiyestahili kuishi.*

*Damu yake ndiyo sadaka ya wokovu wetu,*
*kwa kuwa alikubali kwa upendo abebe na kuondoa dhambi za wote,*
*akimuomba Baba atusamehe.*

*Tunapenda kuweka kila mahali ishara ya msalaba,*
*ukumbusho wa jinsi alivyokubali kutundikwa kwa ajili yetu,*
*lakini sasa hayupo tena msalabani wala kaburini:*
*amekuwa hai tena, anaishi na kutawala milele.*

*Mungu amemfufua kwa sababu Yesu ni Mwanae aliyemtii kabisa*
*hata akajitoa mhanga kufidia uasi wetu.*
*Ndiye njia, ukweli na uzima:*
*hakuna aendaye kwa Baba asipompitia yeye.*

*Kwa sasa hatumuoni,*
*lakini siku moja tutakwenda anakokaa*
*pamoja na Baba na Roho Mtakatifu,*
*akitungojea pamoja na Mamaye na watakatifu wote.*

*Sisi tunaweza kusema na Yesu kwa kuwa yu hai:*
*anatuona, anatusikia, anatupenda, anatusaidia*

*na kutufanya tuwe wema.*

*Kutoka kwa Baba ametutumia Roho Mtakatifu,*
*tusije tukabaki katika ukiwa na hofu,*
*bali tuweze kupendana kama alivyotupenda,*
*na tuwe na umoja kama Baba na Yesu walivyo na Umoja.*
*Roho Mfariji anakaa ndani mwetu,*
*akitutakasa, akituangaza na kutuboresha,*
*tuweze kufanya na kusema mema yote anayotushauri.*

*Anatukusanya katika Kanisa,*
*familia kubwa ya watoto wa Mungu ambao tumemuamini Yesu*
*na kuoshwa dhambi zetu*
*kwa jina la Baba, na la Mwana na la Roho Mtakatifu.*

*Anatuunganisha na Yesu na kututia nguvu*
*ya kuendeleza kazi yake mpaka mwisho wa dunia,*
*kwa kueneza haki, huruma na amani kati ya watu wote,*
*na kwa kuwafundisha, kuwatakasa na kuwaongoza*
*wafikie uzima wa milele.*

*Mwishoni mwa dunia, Yesu atakaporudi kwa utukufu,*
*Baba atawafufua kwa mfano wake wale waliomfuata*
*kwa kupenda wote na kusaidia maskini na wanyonge.*

*Ndipo tutakapofikia ile heri tunayoitamani moyoni tusijue ikoje:*
*heri ya kumuona Mungu jinsi alivyo na kufanana naye milele yote,*
*kwa njia ya Kristo, Bwana wetu. AMINA. ALELUYA.*

## 4. UAMUZI WAKO

*Ndugu,*
*sasa njia iko wazi mbele yako.*
*Huna la kujisingizia, kwa kuwa Mungu amekuandalia na kukujulisha;*
*tena, anakuvuta moyoni uifuate usisite.*

*Huna budi kuamua ama uendelee kumchukiza kwa maisha ya dhambi*
*hadi utumbukie mateso ya milele,*
*ama umkimbilie kwa njia ya Mwanae mpenzi Yesu Kristo,*

*uzidi kumjua na kumpenda kama mtoto mwema,*
*ukishiriki uzima wake bila ya mwisho.*

*Huwezi kusema yuko juu mno,*
*kwa kuwa amekutafuta na kukukaribia kabisa.*

*Anapiga hodi katika maisha yako,*
*ayaongoze kwa Roho Mtakatifu*
*mawazo, maneno na matendo yako yote,*
*umpendeze kama Yesu, Maria na umati wa watakatifu.*

*Kwa neema yake sasa unaweza tu.*

*Jiaminishe kwa Yesu kwa unyofu wote, jinsi ulivyo,*
*pamoja na udhaifu, ujinga na uovu wako,*
*kwa kuwa alikupenda hivi hata akajitoa kwa ajili yako pia,*
*usiendelee kuwa mtumwa wa Shetani.*

*Uwe na hakika kuwa atakupokea tu,*
*kwa kuwa amekulipia msamaha wa Mungu,*
*utakaswe dhambi zako kwa damu yake,*
*uimarishwe na Roho wake,*
*ulishwe mwili wake*
*uzidi kuwa na uzima tele.*

*Hata ikikubidi kujaribiwa kwa namna mbalimbali,*
*utazidi kufurahia amani moyoni na maishani,*
*kwa kuwa baraka ya Yesu itakufuata daima,*
*tena mwenyewe ataishi ndani mwako sikuzote.*

*Basi, ukitamani kuwa mtoto wa Mungu kweli,*
*uwahi kujiunga na familia yake ya kimataifa,*
*ya jana, leo na kesho, ya duniani na mbinguni pia.*

*Katika Kanisa Katoliki hutakuta watakatifu tu,*
*wala usiwadai wenzako wawe wakamilifu tayari,*
*lakini utapata ndugu wa kuongozana nao,*
*na kati yao waandamizi wa Mitume wa Yesu*
*ambao wakupatie mafundisho, ibada na maongozi kamili,*
*kadiri unavyohitaji na kuelezwa zaidi hapa chini.*